Gideoni



Utangulizi

Juma hili tutaendelea kujifunza katika kitabu cha Waamuzi. Mwamuzi mmoja wapo ni Gideoni. Juma hili tutaangalia sehemu ya kwanza ya historia yake na tutaendelea Juma lijalo. Tunapata simulizi ya wito wake katika kitabu cha Waamuzi 6:11-40. Pointi kuu ni

- Mungu anatuona tofauti na jinsi tunavyojiona.
- Kamwe Mungu hawaachi watu Wake
- Mungu anatuita tutimize kazi aliyotuandalia
- Hatupaswi kuogopa Mungu akiwa upande wetu

Video playlist

Muongozo wa Somo

Waulize watoto kama wanakumbuka jina la mwamuzi aliyemsaidia Baraka. Waelezee kwamba muda umefika wa mwamuzi mwingine (mpya), Mungu alimuita mwanamume aliyeitwa Gideoni. Mkumbushe mtoto kazi ya mwamuzi.

Zungumzia namna ambavyo Gideoni aliogopa kufanya kazi ambayo Mungu alimpatia. Zungumzia kipindi ambacho wewe na mtoto wako mliogopa. Fafanua namna ambavyo Mungu atatupatia nguvu tunazohitaji ili kuweza kutimiza kazi aliyotupatia kufanya. Ili kuonyesha, mwaga kifusi cha mchanga katika eneo la nyumbani kwako. Waambie watoto wasafishe mchanga kwa kutumia mikono yao tu. Kama watoto watashindwa au wakivunjika moyo/wakikata tamaa, chukua machini ya kusafishia na kwa pamoja toeni mchanga. Waeleze namna walishindwa kufanya kazi hiyo kwa nguvu zao wenyewe, kama ilivyokuwa kwa Gideoni, asingeweza kufanya kazi aliyopewa na Mungu bila msaada wa Mungu. Zungumzia namna ambavyo Mungu anatuandaa/anatufanya tayari kufanya kazi tunayopaswa kufanya kama jinsi ambavyo unawapatia watoto wako vifaa vya kazi (fagio na zoleo la uchafu). Karirini Waamuzi 6:12, “Malaika wa Mungu alimtokea Gideoni na kusema, ‘Bwana yu pamoja nawe, ee shujaa mkuu’” Mkumbushe mtoto aseme mstari huo kila anapopatwa na hofu/woga, wanaweza kukariri (sehemu ya pili tu ili kufanya mfupi).

Zungumzia kuhusu namna Mungu anatuona tofauti na tunavyojiona. Soma 1 Samweli 16:7b. Elezea kwamba Mungu anaona mioyo yetu. Badilisha maboksi mawili ya biskuti bila mtoto wako kuona. Ingekuwa vizuri zaidi kama biskuti zitakuwa na ladha zaidi kwa ajili ya watu wakubwa na nyingine iwe na ladha ya watoto zaidi. Pia unaweza kutumia viburudisho vya aina nyingine kutoka dukani (vilivyoweka kwenye boksi). Onyesha namna ambavyo kwa nje boksi linaonyesha limejaa viburudhisho lakini kwa ndani linaweza kuwa na matunda. Japokuwa tunaweza shangazwa kukuta aina nyingine ya biskuti ndani ya boksi, lakini siku zote Mungu anafahamu ni nini kipo ndani ya boksi na ndani ya mioyo ya watu.

Waeleze namna ambavyo Mungu hawaachi watu Wake. Wafafanulie maana ya kuacha ni kutelekeza (bila kujali kitu), lakini kamwe Mungu hatuachi peke yetu/hatuachi wapweke. Waelezee kwamba, japokuwa hatumwoni Mungu, lakini siku zote yupo. Kama kuna chumba kisicho na dirisha, nendeni ndani ya chumba hicho. Washike watoto wako mikono na kisha uwashe taa. Japokuwa haukuwaona sababu ya giza, lakini bado walijua upo pamoja nao ndani ya chumba hicho. Wakumbushe kwamba Yesu alituahidi akisema, “Siku zote nitakuwa pamoja nawe,” (Mathayo 28:20). Furahini kwamba ikiwa tunaye Yesu mioyoni mwetu, basi kamwe hatuwezi kuwa wapweke.

Muombeni Yesu awasaidie siku zote kufanya kazi Yake aliyowaambia mfanye na wala msiogope.

© 2023 truewaykids.com

Mungu alimwahidi Gideoni kuwa atakuwa pamoja naye.

Mungu alimpatia Gideoni ishara ili kumuonyesha kwamba Yeye hutunza ahadi.

Gideoni alimwamini Mungu. Aliwaambia watu wamtii na kumpenda Mungu.

Gideoni

Watu walimsahau tena Mungu

Kila mwaka adui alikuwa nchini mwao na kuiba wanyama na chakula chao.

Hilo liliwafanya watu kuwa na huzuni sana. Walimuomba Mungu msaada.

Gideoni alikuwa bado ni kijana wa Israeli. Alikuwa ni mkulima anayelima ngano.

Gideoni alijificha pangoni ili apepete ngano.

Alikuwa anawaogopa maadui.

Hakutaka waibe chakula.

Mungu alizungumza na Gideoni.

Mungu alimwita Gideoni shujaa mkuu.

Hakujiona kama shujaa mkuu. Alikuwa anaogopa sana.

Alikuwa ni mdogo katika familia yao.

Shughuli na Michezo

Kujificha na kutafuta

Waelezee namna ambavyo Gideoni alijificha katika pango ardhini sababu ya maadui.

Fanya mchezo wa kujificha pamoja na watoto wako. Hesabuni kuendana na uwezo wa watoto wako.

Majaribio ya Unyevu au Kavu

Ili kuelewa majaribio ya Gideoni, weka kitambaa cha jikoni sehemu tofauti na uangalie ni nini kitatokea.

Waulize watoto wako kama kitabaki kama kilivyo, kikavu au kitakuwa na unyevu, wabunie jibu.

Mchezo wa unga

Weka kiasi cha unga katika trei. Waeleze kwamba tunapata unga wa ngano kutokana na ngano.
Waeleze watoto wako wachore au waandike namba au herufi katika trei ulilowekа unga wa ngano.
Unaweza kutengeneza herufi ili waweze kuiandika kama ilivyo.
Ili kufanya mchezo uwe wa kuvutia zaidi, wanaweza kumaliza kucheza kwa kucheza na wanasesere wa magari ya kuchimba, wachimbe katika unga.

© 2023 truewaykids.com

Gundua utofauti

Vitu 6 vya kutafuta

© 2023 truewaykids.com

© 2023 truewaykids.com

Mtafute Gideoni na wanyama







Mchezo wa mzingile

Msaidie Gideoni apate njia ya kurudi bandani akiwa na ngano.

© 2023 truewaykids.com

Unyevu au Kavu

Chora mduara kuzunguka watoto waliolowana/ wenye unyevu.

© 2023 truewaykids.com

Blanketi la Ngozi

Mahitaji:

- Vipande 2 vya A4 vitambaa
- Pamba/sufu/manyoya ya kondoo
- sindano ya plastiki au yenye usalama
- mikasi
- kalamu ya felti

https://youtu.be/HmJU-FHXdcI

Nini Kifanyike:



Kunja kitambaa ili kufanya pua ndogo nje ya kitambaa ambacho utatumia kuwazungushia uzi wa pamba au sufu.



Tumia sindano ya plastiki na baadhi ya sufu; tumia blanketi pembezoni mwa kitambaa.

Endelea hadi utakapomaliza urembo wa pembeni. Funga mwisho wa kamba kwa pamoja.



Chora namba ya mwanasesere wa watoto wako katika nguo nyingine ya rangi.

Kata herufi na urembo mwingine na ubandike katika blanketi.

Ruhusu ikae kwa muda ili gundi ikauke.

© 2023 truewaykids.com

Paka picha rangi

Kata mistari ya vidoti na kamba ya manyoya au Ngozi.

zungusha kamba sehemu ya mstari wa vidoti.





https://youtu.be/rjle9k4SaHw

© 2023 truewaykids.com



© 2023 truewaykids.com

© 2023 truewaykids.com



© 2023 truewaykids.com



© 2023 truewaykids.com

Muda wa kuabudu

Agiza kuimba wimbo wa kuabudu. Siyo ulioandaliwa na Trueway Kids.
Video za Yutube zitumike kwa matumizi binafsi tu.

Be bold, Be strong

https://youtu.be/zRvCUz6KFB4

Mighty Warrior

https://youtu.be/CCEtqL7HTZQ

I Won't Be Afraid

https://youtu.be/YhAH2zU8UiU

Muda wa maombi

Mshukuru Mungu kwa kuwa anawasamehe watu

Muombe akusaidie usiwe unaogopa bali umwamini Yeye.

Muombe Mungu akusaidie ujione/ ujitambue wewe ni nani Kwake.

Juma lijalo

Jeshi la Gideoni la watu (wanaume) 300

Kama bado hujafanya hayo, jiunge kwa barua pepe ili kupokea somo la wakati ujao.
truewaykids.com/subscribe/

© 2023 truewaykids.com